Cambridge Assessment International Education

# Cambridge IGCSE™

**SWAHILI** **0262/02**

Paper 2 Listening **May/June 2022**

TRANSCRIPT **Approximately 45 minutes**

This document has **8** pages.

© UCLES 2022



https://xtremepape.rs/

Eng: Cambridge Assessment International Education
Cambridge IGCSE in Swahili
Paper 2 Listening, May/June 2022
Turn over now

*(Pause 5 seconds.)*

TLR: **Zoezi 1**

TLR: Utasikia vipande vinane vifupi vilivyorekodiwa.
Jibu swali la 1–8 katika nafasi uliyopewa.
Majibu yako yawe mafupi iwezekanavyo.
Utasikia kila rekodi mara mbili.

TLR: Swali 1

M: * Vipi Asha, uko wapi?

F: Nipo nyumbani, kwani vipi?

M: Hujatoka hadi sasa? Mbona utachelewa sana?

F: Nitachelewa kufanya nini?

M: Umesahau leo ni harusi ya Juma na Roza?

F: Hivi ni leo? Siwezi kuwahi hata nifanyeje. Watasikitika sana!

M: Nenda tu hata ukichelewa si vibaya.

F: Sawa. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 2

M: * Hivi umesikiliza nyimbo mpya ya mwimbaji kutoka Tanzania anayeitwa Chege G?

F: Mimi ni shabiki mkubwa sana wa Chege G. Nimeshakariri nyimbo yote tangu juzi!

M: Alaa kumbe! Hivi unampendea nini hasa mwimbaji huyu?

F: Maneno na mdundo wa muziki wake unanivutia sana.

M: Hivi kuna chochote usichokipenda kwake?

F: Labda niseme kwamba mimi sivutiwi na nyimbo zake za Kiingereza au Kilingala. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*



https://xtremepape.rs/

TLR: Swali 3

M: * Tangazo! Basi linalotoka Nairobi litafika hapa kituoni leo saa kumi jioni. Basi linalotoka Mombasa litachelewa kwa dakika arobaini na tano kutokana na hali mbaya ya barabara. Basi lililopo kituoni hivi sasa ni lile lililotoka Nakuru. Basi hilo halitachelewa na litaondoka kurudi Nakuru baada ya nusu saa. Wasafiri wote wanasisitizwa watazame ratiba ya usafiri inayoonyesha mabadiliko yote. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 4

F: * Maprofesa watatu wameandika vitabu muhimu kuhusu maisha ya mwalimu Nyerere, baba wa taifa la Tanzania. Vitabu hivyo vimechapishwa ili kuadhimisha miaka mia moja tangu kuzaliwa kwake. Ni vitabu muhimu ambapo kwa mara ya kwanza maisha yote ya Mwalimu Nyerere yamejumuishwa. Kwa wale wanaofikiri kwamba wanamfahamu vizuri kiongozi huyu wa zamani, watashangaa kusoma visa vingi vipya ambavyo havikujulikana hapo awali. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 5

M: * Jina langu ni Anil. Kweli nimeamini kwamba miaka inavyoenda ndivyo tunavyozidi kubadilika. Mimi nilikuwa mpenzi mkubwa wa kucheza dansa. Nilikuwa sikosekani kwenye viwanja vya muziki. Siku hizi, siku pekee ninazoweza kukaa macho ni siku za sherehe kama mwaka mpya na harusi kwa sababu ninapenda kutazama fashifashi. Raha yangu sasa ni kula chakula kizuri migahawani na kulala mapema kwani usingizi ndiyo raha ya maisha yangu. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 6

F: * Hongera kwa washindi wa shindano letu la ushairi ambao wametuambia kwamba kuwaona washairi wao wapendwa kwenye televisheni ilikuwa kama zawadi kwao. Bila shaka mtafurahia matunda ya ushindi wenu kwa kujipumzisha kwenye fukwe za bahari kwa siku chache. Washindani wa shindano la mwezi ujao wajitayarishe kwa kununua nguo za kuogelea pia ikiwa watapata bahati ya kushinda. Tunawatakia kila la heri. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 7

M: * Habari za jioni, hapa ni ofisi ya ngome kongwe, nikusaidieje?

F: Nzuri, asante. Nilikuwa ninataka tiketi tatu kwa ajili ya maonyesho ya taarabu ya leo usiku. Je, kuna nafasi viti vya mbele?

M: Zimebaki tiketi chache sana na zote ni za kusimama, hakuna tiketi za viti vya kukalia.

F: Hiyo itakuwa shida sana kwangu. Kutakuwa na maonyesho kesho?

M: Ndiyo, na viti vipo.



https://xtremepape.rs/

F: Basi, afadhali. Ninataka kununua tiketi tatu tafadhali, kwa kesho. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 8

F: * Tumekodi chumba kwenye hoteli iliyo nje kidogo ya mji. Kulikuwa na chumba cha watu watatu ambacho kilikuwa na kiyoyozi, pia choo kilikuwa ndani. Bei ya chumba hicho ilikuwa ghali zaidi ya chumba tulichokichagua ambacho kina feni. Uzuri ni kwamba choo kipo ndani pia. Kwa vile tutazurura sana, sikudhani kama kulikuwa na haja ya kulipa zaidi. Pia hoteli itatupa mataulo na mashuka masafi kila siku. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 1. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 2. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 2.

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: **Zoezi 2**

TLR: Utamsikia Rachel anazungumza kuhusu utamaduni wa kusoma.
Msikilize na malizia sentensi.
Andika neno moja au maneno mawili tu katika kila nafasi.
Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Hivi karibuni nilisoma makala iliyoelezea kwamba vijana wanapenda sana kusoma ingawa, kwa uhakika, wao hutumia muda wao mwingi mbele ya skrini tofauti. Makala hiyo ilidai kwamba, kutokana na utafiti uliofanywa na chuo kikuu kilichopo mjini kwetu, vijana wengi husoma kwa sababu wanataka kufanya hivyo ili kufaulu masomo yao na si kwa sababu tuna utamaduni wa kusoma.

F: Lakini pia, makala ilielezea kwamba kuna vijana wengi ambao husoma wakati wao wa mapumziko. Mara nyingi vijana hawa hupendelea kusoma vitabu vyao wanapokuwa katika sehemu zenye faragha kama chini ya vivuli vya miti, sehemu za starehe kama ufukweni mwa bahari na hata vyumbani mwao.

F: Pia vijana husoma vitabu tofauti ikiwa ni pamoja na fasihi. Fasihi wanazozipenda zaidi ni zile zisizo na uhalisia kwa hivyo hutumia mandhari za kufikirika. Vijana wengi husoma vitabu na pia fasihi tofauti mtandaoni. Kwa kawaida hizi huandikwa na waandishi chipukizi ambao huziandika kwa lengo la kutafuta kampuni za kupiga chapa kazi zao. Hata hivyo, vitabu vya waandishi mashuhuri pia zipo mtandaoni kwa bei rahisi.

F: Utafiti umeeleza kwamba vijana husoma kwa muda usiopungua saa tatu kwa wiki. Wao hutumia muda wa saa tano kwa wiki kwenye matumizi ya intaneti. Kwa hivyo, ni kweli kwamba muda mchache zaidi hutumika kusoma kuliko ule unaotumiwa kudurusu tu. Pia, ingawa wazazi hufikiri kwamba watoto wao huingia mtandaoni kutafuta njia za kupakua nyimbo zisizo na malipo na filamu za kisasa, ukweli ni kwamba wengi husoma pia.

F: Makala hiyo ilielezea jinsi tabia ya kusoma inavyoathiriwa na mazingira ya vijana. Wale vijana ambao wanavutiwa sana na kusoma ni wale ambao wazazi wao pia ni watu wanaopenda kusoma. Mara nyingi vijana hawa husomewa au husimuliwa hadithi wanapokuwa watoto. Wanapokua, wao huvutiwa na kujisomea.



https://xtremepape.rs/

F: Kwa wale ambao hawana uwezo wa kupata vitabu kirahisi, hasa kutoka madukani, kuna umuhimu wa kukuza maktaba nchini kwetu. Kwa hivyo ni lazima kufikiria jambo hili ili watoto wote waweze kusoma nyumbani. **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Pause 3 seconds. Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 2. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 3. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 3.

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: **Zoezi 3**

TLR: Utawasikia watu sita wakizungumza kuhusu mawasiliano.

Oanisha wasemaji na mawazo katika orodha A–G. Kwa kila msemaji, andika herufi (A–G) katika mstari wa jibu.

Tumia kila herufi mara moja tu. Kuna herufi ya ziada isiyohitajika.

Utasikia rekodi mara mbili.

TLR: * Msimulizi 1

F: Mtu anavyoyaitikia maneno anayoambiwa ni muhimu sana katika mawasiliano. Ukiona mtu anasita au anakukwepa kwa kuangalia kwengine kama sakafuni au anajaribu kubadili mada basi ujue huyo mtu hapendi unachoongelea au hakusikilizi. Yule anayetabasamu au kuitika kwa kichwa anakusikiliza na anakubaliana na wewe. Mimi ninapendelea zaidi kuzungumza na watu ili nielewe wanavyohisi kuhusu yale tunayoongelea. Wenzangu huniuliza kwa nini situmii barua pepe kuwasiliana au hata kutuma ujumbe, ukweli ni kwamba sina subira kabisa.

TLR: Msimulizi 2

M: Ninapokwenda safarini, mimi huwatumia ujumbe wa maandishi rafiki zangu. Lakini njia ya mawasiliano iliyo rohoni mwangu ni kuandika barua na kuituma kwa njia ya posta. Hii inahitaji mtu asiwe na haraka kwani inabidi kuwa na karatasi inayovutia, kalamu, bahasha na stempu. Tena mimi hunyunyizia marashi kabla ya kuituma. Mtu anapoipokea anahisi kweli aliyemtumia anamjali. Pia ni kama kuzungumza na mtu uso kwa uso. Kuandika postikadi pia kunavutia lakini huwezi kuandika jambo la siri kwani yeyote anaweza kuzisoma.

TLR: Msimulizi 3

F: Barua pepe ni njia ya mawasiliano rahisi kuliko zote. Unaweza kumwandikia yeyote na taarifa inamfikia haraka. Barua ya kawaida inachukua muda mrefu kumfikia mlengwa na tena inaweza kupotea njiani. Njia niitumiayo hasa ni kutuma ujumbe mfupi. Nimegundua kuna mitandao mingi ambayo inatoa huduma hii bure, tena humfikia unayemwandikia hapo hapo, ni kama barua pepe lakini bora zaidi. Pia unaweza kuona alama inayokuonyesha kama mlengwa ameufungua ujumbe au la.



https://xtremepape.rs/

TLR: Msimulizi 4

M: Kifaa changu cha mawasiliano kilipasuka wiki iliyopita. Mama yangu ameniazima kompyuta yake ili niwaarifu rafiki zangu kuhusu janga lililonikumba. Nilifungua barua pepe yangu ili niwaandikie halafu nikaikumbuka njia ya mawasiliano ambayo nimeipenda tangu utotoni. Papo hapo nilikimbia mjini na kununua postikadi halafu nikawaandikia wote. Wengine wamenijibu kwa njia hiyo hiyo na kuniambia walishasahau starehe ya kupokea postikadi. Ila kuna wengine naona wameshasahau jinsi ya kuandika maana maandishi yao yana makosa! Inavunja moyo kweli.

TLR: Msimulizi 5

F: Ninapokuwa kazini mimi hubandika vijikaratasi vyenye taarifa katika sehemu tofauti. Hii ni tabia ambayo imeendelea tangu utotoni kwani nilipenda sana kuwaandikia postikadi majirani ili kuwaarifu mambo ya mtaani. Hivi karibuni nimegundua njia ya kuwasiliana nitakayoitumia milele. Ni njia ya video. Inafurahisha mno kuwaona wenzangu walivyo na pia sehemu walipo. Ni kama tunazungumza uso kwa uso. Ajabu ni kwamba kuna watu wengine hawapendi video na ninapowasiliana nao hawapokei. Hii hunihuzunisha na mimi huwaarifu kwamba nilikuwa ninataka kuwasalimia tu.

TLR: Msimulizi 6

M: Watu wanaopenda kuwasiliana kwa kutumia video hukera sana. Hutaka kuzungumza asubuhi wakati wanajua wenzao wamechoka na labda hawana furaha. Tofauti na ujumbe ambapo mtu anaweza kuona kama umepokea, njia ya video haionyeshi kama mtu ameiona, kwa hivyo huwa sijibu tu. Barua pepe ndiyo njia ya kisasa ya kuwasiliana, hasa kazini. Unaweza kujibu unapotaka, na hulazimiki kutabasamu. Watu wote wangetumia njia hii maisha yangekuwa mazuri. Siwaelewi watu wanaoandika barua kwa kalamu. Jambo hilo limepitwa na wakati. Taarifa wanazoziandika unakuwa umeshazipata kabla hata hizo barua kukufikia. **

*(Pause 5 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 3. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 4. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 4.

*(Pause 30 seconds.)*



https://xtremepape.rs/

TLR: **Zoezi 4**

TLR: Utasikia mazungumzo kati ya Hannah na Amin.

Sikiliza mazungumzo hayo na soma maswali.

Kwa kila swali chagua jibu sahihi kati ya A, B au C.

Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi.

Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Hivi Amin, umesikia habari yoyote kuhusu pendekezo jipya kuhusiana na lile pori nje ya mji?

M: Ndiyo. Nimesikia wanataka kujenga nyumba katikati ya pori. Unajua kama ingekuwa nyumba kumi au hata ishirini, mimi nisingekuwa na tatizo sana. Lakini nyumba mia mbili? Tena nyumba zenyewe ni nyumba za likizo ambazo hazina ulazima kabisa. Hapo si kama wanajenga mji mpya tu? Tena mji usiohitajika maana utatumika mara moja moja! Tena labda baadaye watasema itabidi kujenga na jumba la muziki au starehe zingine ili watu wapate kazi. Mimi sikubaliani kabisa na wazo lao na nitalipinga kwa hali na mali.

F: Hata mimi nina wazo hilo pia. Lakini tutafanyeje?

M: Kwanza tutawaambia wahusika historia yetu na pori lile. Unajua mimi nilianza kuja maeneo haya zamani nilipokuwa mtoto wakati wa likizo. Wazazi wangu walikuwa wanafanya kazi wakati shule zimefungwa na mimi nilikuwa ninakuja hapa kupumzika kwa bibi na babu yangu. Mara nyingi nilikaa mwezi mzima. Nilikuwa nahisi sina wajibu mwengine zaidi ya kuchunguza na kucheza nilipokuwa porini humo. Ilikuwa raha sana.

F: Kumbe? Sikujua! Ilikuwaje wakati huo?

M: Hili pori kama unavyolijua ni kubwa mno. Wakati ule hata njia unazoziona sasa hazikuwepo. Hizi zilizokuwepo sasa hazikuchimbwa na serikali, ni matokeo ya watu kama sisi kutembea humo kila mara. Mimi na babu yangu tulipenda kutembea na kusimama kila baada ya dakika chache tukitazama majani na mizizi ya miti tofauti. Mwanzoni mimi sikuwa na subira ya kuielewa miti na mimea na nilipenda kutembea haraka haraka, lakini miaka ilivyoenda, niliweza kuifahamu ndani nje, nje ndani. Nilipatana zaidi na babu yangu na tulishinda tukizungumza na kunusa maua huku tukichunguza mizizi ya miti.

F: Ndiyo maana unaijua vizuri sana. Kumbe ni urithi wa babu yako. Yeye alikuwa mtaalamu wa mimea?

M: Hapana, yeye hakuwa mtaalamu, alivutiwa tu na mimea. Babu yangu alijifunza majina ya miti yote na alinifahamisha ipi ilikuwa dawa na ipi ilikuwa sumu. Alipenda sana ukimya uliokuwapo huko porini pamoja na hewa yake safi. Unajua, ingawa watu wengi huenda porini, si kawaida kukutana na watu unapokuwa humo. Sijui kwa nini. Kwa hivyo tulijihisi kama tupo peke yetu duniani na pori lile lilikuwa kama letu.

F: Itabidi kuandika yote haya unayonielezea. Kwa njia hiyo, wahandisi waliotumwa hapa wataelewa umuhimu wa pori hili kwetu sote.

M: Kabisa. Pia tulichuma mboga ambazo tulizichukua nyumbani na kuzipika, kwa mfano mchicha pori unaoota katika pori lile ni mtamu ajabu. Hadi leo mimi huenda kuuchuma. Watu wengi hawaufahamu. Pia tofauti na watu wanavyofanya hivi sasa ambapo wengine huogopa matunda pori na wengine hula kidogo kule kule porini, sisi tuliyachuma na kuyabeba hadi nyumbani



https://xtremepape.rs/

ambapo tuliyaosha na kuyala. Babu yangu alipenda kuwagawia majirani zake matunda aliyoyachuma porini pia.

F: Siku moja ukinialika kwako nitafurahi kama utanipikia mchicha huo. Sijawahi kula mchicha pori.

M: Basi tutapanga hivyo. Unajua uzuri wa hili pori ni kwamba familia zinaweza kuja kutembea na kuwa pamoja huku wakifurahia hewa safi, wakizungumza na kuwa kwenye mazingira safi. Pori ni tofauti na bustani kubwa za umma ambapo watoto wanaweza kuenda na kucheza mpira au kukimbizana huku wakipiga kelele. Humu ndani si pa kukimbizana na kucheza mpira. Ingawa serikali haijaweka bango linalokataza kucheza lakini watu wanasaidiana kufahamu kuwa kuna mfumo wa kiikolojia ambao watakuwa wanausumbua wakifanya fujo. Hebu fikiria kama watoto wakirusha mipira kwenye miti itakuwaje?

F: Kweli. Kuna aina nyingi za wanyama wadogo na ndege ambao watakuwa wanawasumbua.

M: Kabisa. Pia pori likikatwa wanyama hao watapoteza malazi yao. Hebu fikiria sungura, mbweha na hata nyoka tofauti wanaoishi humu. Maisha ya wanyama yataharibika pia. Kuharibu maisha ya viumbe kama hivi ndiyo njia moja wapo ya kuongeza joto joto la dunia.

F: Basi itabidi tukutane ili tuzungumzie mipango ya kufanya.

M: Kama una muda, njoo nyumbani kwangu kesho saa nane mchana. Nitakupikia mchicha pori.

F: Asante sana. Tutaonana kesho. **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 4, na mwisho wa mtihani.

Eng: That is the end of the examination.

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge Assessment International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge Assessment International Education is part of Cambridge Assessment. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which is a department of the University of Cambridge.

© UCLES 2022



https://xtremepape.rs/